

PASUA KICHLWA

© Muddyb Mwanaharakati

Kimechapwa na;
Dar General Publishing House,
Dar es Salaam,
Simu: 0713538427.

Mhariri: Luah Sanaa
0672-632-815

Jalada: Kindo Emmanuel
Frank Masai
0623-329-822

ISBN:978- 9976- 5467- 4- 3

© *Muddyb Mwanaharakati, 2021*
Mobile: 0713538427

Chapa ya kwanza, **2021**

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kupiga chapa,
kutafsiri au kikitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya
maandishi kutoka kwa Muddyb Mwanaharakati.

SHUKRANI

Shukrani faafu ni kwa Mungu baba aliyenipa kipawa hiki cha kuandika na uhai. Mama yangu mzazi kwa kunileta duniani leo hii—Mola akupe kauli thabiti huko uliko. Kila siku nakuombea dua, mama'ngu! Ningependa kuwashukuru marafiki zangu wa karibu waliosoma riwaya hii ikiwa katika hali ya muswada kabla hata kufikiria kama hili lililotokea sasa lingetokea. Marafiki zangu hao ni pamoja na Diana Ruta, Jamila Kimoto, Bupe Shemgaa, Winfrida Magawa, Magreth Peter, Molio Baldwin, Ntila Mabambazi, Mayna Pemba, Zamira Sanguti, Rashind Sengwira, Buinda Mjungu, Hellen Chris, Salim Al Jabry, Godfrey Makaranga na wengine wengi tu.

Pia ningependa kumpa shukrani za kipekee kabisa rafiki na mdogo wangu Luah Sanaa kwa kuusoma mswada huu mara mbili na mwisho kurudi na jibu kamili. Muda wako ungeweza kutumia kwa mambo mengine lakini uliona kuna haja ya kutazama maandishi ya kaka yako kama si kijana mwenzako. Kwa hili, sina neno ambalo naona lingefaa kuliweka ili kuelezea shukrani zangu kwako. Mungu akusimamie kwa kila ultendalo mdogo wangu.

Kaditama, ninadiriki kusema ninawapenda wasomaji wangu wote mnaonifuatilia kule Facebook na mitandao mingine. Mmekuwa chachu ya kunifanya niendelee kuandika kila siku bila kuchoka. Ninawaahidi sitachoka kuandika hadi dakika ya mwisho.

Shukrani za mwisho ziwaendee wanachama wenzangu wa READING MARATHON. Ahsante sana. Ninawapenda.

Mohamed Lupinga (Muddyb)

Chanika, Dar es Salaam,

30 Januari, 2021—Jumamosi.

Saa tisa na dakika arobaini alasiri.

PASUA KICHWA

SEHEMU YA KWANZA

Usiku ulikuwa ukijongea, ukazalisha nuru ya kutosha angani yenye kumetameta na kuvutia. Wakati mwanga unakunja sura, kuna sehemu pia kulikuwa na watu wakikunjua pendo lao bila wasiwasi. Hawana habari. Maadamu mioyo yao imeamua kujifariji mahali walipokuwa. Chimbo hilo la hatari, alikuwapo Agness na kijana maarufu mwuza madafu mwenye jina la Boy. Wakiwa katika harakati zao chimboni, kwa mbwembwe na huba la wizi Agness akasema, "Unajua ni muda gani nilikuwa n'nakufuatilia we' Boy?" akamtupia na jicho lililogeza kupita kiasi. Laiti kama ungelikutana nalo, basi ungelisema Agness alikuwa katika kilele cha nafsi kuachana na mwili wake.

"Hapana! Sijui kabisa, madam!" Boy alijibu, lakini kwa kititemeshi. Agness akaanza kukunja na kukunjua kishati kilichomshika sana Boy. Vijana wa kileo wanakiita, kimodo! Akiwa katika kagale hiyo akasema, "Acha kuuza madafu bwana! N'takupangia chumba!" sauti yake kimahaba ilisikika mithili ya mtu aumwaye mafua. Ikawa kilainishi cha moyo wa kijana huyo mchakarikaji mtaani hapo.

"Chumba?" Boy alihoji kwa mshituko huku akirudi nyuma. Agness hakuzubaa. Akaunganisha na jibu lake, "Chumba ndio! Ajabu kitu gani kwani?" alijibu kwa uchangamfu huku akimtazama usoni. Kijana Boy akashikwa na mtanziko kiasi. Hakuelewa mantiki ya kuambiwa aache kujitafutia mkate wake wa kila siku, abaki nyumbani, apangiwe chumba halafu? Likamtoka swalii.

"Kwa hiyo n'takula chumba kwa kuacha kazi ya madafu au namna gani? Hapo sijakuelewa, madam!" alijibu huku akitoa jicho la shauku ya kutaka kujua kusudio la Agness. "We' na we! N'nakupangia chumba ili kukupunguzia matatizo, na tuwe huru tukitaka kufanya yetu. Ukiwa nacho naweza kuja muda wowote

katika chumba chako!" Agness alisema huku akibirua gololi za macho yake kimahaba mno.

"Na yule bwana'ko je?" Boy alihoji kwa kihoro. Bila aibu, Agness akajibu.

"Yule ana mkewe, kanipa nyumba nzima, na karibia kila siku n'nalala mwenyewe hadi atakapojisikia nd'o aje." Hakuishia hapo, Agness akasafirisha kiganja cha mkono wake kifuanani kwa Boy aliyebananishwa kwenye ukuta kichochoroni kama mwizi. Ushindani mkubwa wa pumzi zake ulikuwa ukisikika kupitia mihemo aliyokuwa akiitoa. Kutokana na urembo aliokuwa nao Agness, halafu Boy akajitafakari kazi yake, kupendwa au kubananishwa ukutani na mtoto mzuri kama Agness, akili yake haikuweza kuchangamana kati ya ujinga wake na utimamu.

"Hebu, Madam, naomba niwache kidogo nipate pumzi." Boy alisema huku akitweta kwa wahaka. Dhihaka? La hasha!

"Nini tena Boy? Mbona unanifanyia hivyo?"

"Hamna, Madam... presha... pre-e-sh-a"

"Imefanya je tena? Ngoja basi... Bo...Boy..!"

Wakati akiongea hivyo, Agness hakusubiri ruhusa kutoka kwa Boy. Akajitia ujuzi wa kusaili visivyo sailiwa. Naam! Kama haitoshi, polepole vidole vya mkono wa kushoto vikizama katika sikio la kushoto la Boy, akawa anavisokota polepole sikioni mwa kijana huyo. Dunia na maajabu yake yakapiga hodi katika mlango wa fahamu wa Boy. Pumzi zake zikaanza kusutana. Jicho likamtoka kupita maelezo. "Kitu gani tena hii?" Boy alilalama nafsini. Hakuweza kujitoa wala kutolewa. Thutbutu yake!

Katika hali isiyo ya kawaida, Boy akaanza kupiga yowe kali lisiloeleweka. Dhamira ya Agness kumkwida kichochoroni bila kutarajia ikaanza kumwendea kombo. Kwa taabu akasema.

"Madam, Madam, utaniua wallah!" kikafutiwa na kihemo cha nguvu. Mawasiliano kati ya akili ya Boy yalizidiwa na hisia jongeshi zilizokuwa zikipita katika mishipa yake ya fahamu. "Madam, mikono yako laini mithili ya su.. su... sufi... we ni mtu

au jini?" Boy alihoji kwa kihoro. Haikuwa bayana kama ni huba au woga ulimtawala. Katika tukio hilo, polepole nguvu zilianza kumwishia. Agness akamjibu Boy swali lake.

"Kwa nini, Boy?" akatoa tabasamu hafifu. "Hujaona kitu bado..." Agness aliongeza huku akimkata jicho la huba Boy wa watu aliyegeea kama anataka kufa.

Mkono ulioenda chumbani kwa babu ulianza kufanya yake iliyokusudiwa. Mambo yaliyotokea huko mvunguni kwa Boy yalipelekea atoe yowe mujarabu. Naam! Akasema, "Nafwa miye leo... We' malaika n'takupeleka wapi miye!" Boy alilombokeza na kauli za majuto kwa kuhofia huenda leo tu, kesho asimhitaji kutockana na mwonekano na hali alonayo Agness! Hakuelewa alitaka nini kwake, pengine hofu ya utofauti wa kihadhi ilipelekea kutojiamini. Hakustahili?

Baada ya sekunde kadhaa ya misukosuko ya nafsi ya Boy, ghafla mkono wa Agness ukatoka na fadhaa! Boy hakuweza kuhimili vishindo vya Agness matokeo yake kaanza kufika Mlima Kilimanjaro kabla hata ya kuvuka Chalinze. Agness akamaka.

"Aaaaah, Boy, jamani kujiendekeza gani huko sasa! Hata sijananihii mara usha..." Kabla Agness hajamaliza kusema, Boy akamrukia Agness katika kifua chake. Akaanza kushika ngogwa kama hana akili nzuri...

"Boy, Boy! Polepole hapa njiani watu wanaweza kupita muda wowote ule..." Agness alisema huku akipiga mhemo usiomithilika. Wakati huo akili zao zishahama. Nusu wanadamu, nusu wanyama.

"Siwezi tena! Siwezi kwa kweli..." Boy alijitahidi kuongea lakini sauti iliyotoka kama una tatizo la kusikia huwezi kumuelewa hata kidogo. Eneo lilikuwa na kiza na muda ulikuwa ushapaa, Agness aliiinka na kumshika mkono Boy akasimama naye kisha akamtazama usoni.

"Nikusaidieje?" Agness alimwuliza Boy.

"Jibu unalo! Tafadhali sina hali!" Boy alijibu lakini macho yake alikuwa kama mtu aliyevuta bangi. Hakuwa na uwezo wa kutazama moja kwa moja. Mawazo ya vichwa viwili yalimwingia hasa. Hakujua kichwa gani kina mamlaka kwa wakati huo. Ibilisi huyu!

"Lakini hapa si salama sana, Boy?"

"Unaongea sana! Ningekuwa 'nshamaliza tayari mwenzako!"

"Jamani, Boy!"

"Kweli, Madam!"

Maneno haya yalipoozesha nafsi ya Agness ikafanya macho yake kuwa kama mwizi. Mara katazama kulia mara kushoto.

"Basi sawa ngoja n'shushe kistiri changu lakini utafute hayo madini ya Tanzanite chapchap, sawa?" Agness alisema kwa msisitizo.

"Sawa. N'tafanya hivyo!" Boy alijibu lakini jibu lake halikutoka na sauti thabiti.

Agness akapiga doria ya mwisho kwa macho kisha akapunguza usitiri wa kivalo na kuinama huku Boy akiwa nyuma yake. Boy naye hakutaka muda umponyoke akasaula upesi tayari kupambana nao huo muda.

Boy suruali ipo kati, akamsogelea Agness akashika sehemu za kati za mwili wake kilichopambwa kwa chachandu za dhahabu. Mwinamo ulioumba umbo la Punda milia. Ile yupo mlangoni kwa bibi tu, wenye mji wa ndani wakatoka nje kabla hata hajaufikia mlango wa bibi Agness.

Hali iliyopelekea kumchafua vibaya mapajani na katika kisitiri chake chote ndembendembe. "Aah jamani, Boy, unanifanya makusudi sasa. Kweli tena? Jamani!"

"Samahani madam! Sio kusudio langu!"

"Imekuwaje? Eh?"

"Mfadhaiko... ulinishika na Muumba naye hakuchoka siku aliyokuumba basi nikashawishika zaidi," Boy alisema huku maneno yakitoka kwa taabu. Maumbo ya sentensi zake hazikomai zikasikika vyema. Kauli na macho haviendani. Taharuki mtindo mmoja. Agness hakuelewa kilichotokea. Ghadhabu! akachutama na kupandisha juu sketi yake ya *jinzi* bila hata kujifuta huku michuzi ya wazungu pori ikichuruzika mapajani. Hakujali. Alikuwa na fundo nafsini.

"Umeniudhi sana, Boy! Yaani, vibaya mno," Agness aliongea kwa manung'uniko huku akipiga konde mkono wake wa kushoto.

"Nisamahe madam! Haitajirudia tena. N'nakuahidi kikwelikweli sasa," Boy alijibu kwa hofu—maana kiwewe alichokipata ni zaidi ya kiwango cha lami .

"Sijakuelewa kabisa. Kweli tena. Dah!" Agness aliongea huku akijitia kukunja sura. Vile urembo ulivyomshika hana umiliki wa kisirani hata nukta moja. Mashindano ya pumzi kuingia ndani na kutoka yalipamba moto. Wasiwasi wa kutemwa ukabisha hodi katika mlango wa fahamu wa Boy. Akasema, "Nisamehe sana, madam. Sikudhani kama safari yangu ingeishia njiani. Tafadhali naomba unielewe!"

Agness aliendelea kujitingisha mwili wake kwa madaha. Hapo alizidisha udeko Boy asiwe na la kusema zaidi. Alibaki kumshika mikono kupoza hasira ya Agness. Ghafla Agness akajitia kujitoa kando kidogo kutoka aliko Boy. Boy hakutia juhudu zaidi za kutaka kumzuia bali alisimama imara huku sura yake ya huruma ishika hatamu.

Piii! piiii! Honi ya gari ilisikika kwa sauti kali mno. Ikarudi mara kadhaa kwa msisitizo wa hali ya juu. Sauti ilitokea upande wa kushoto ambapo ndipo ilipo nyumba ya Agness aliyonunuliwa na shefa lake la Kigogo maarufu bwana Chibago.

Ni mkurugenzi wa shirika lilisilo la kiserikali linalosimamia masuala ya utunzaji wa mazingira ya baharini. Hasa wamejikita katika kuondoa taka za plastiki baharini. Kengele ya hatari ikawaka kichwani kwa Agness. Akasema, "Hiyo itakuwa honi ya gari ya mshefa wangu!" akashusha pumzi kivivu.

"N'tafute ba'dae!" akaongeza huku akiondoka na sketi yake ikiwa bado haikukaa mahali pake vema. Alikimbia miguu iligongana kwa kutetemeka kwa hofu ya kutofungua geti kwa muda unaostahili. Hakuzubaa, alitumia mbio hadi mlango wa nyuma, akafungua geti dogo *upesiupesi* na kuingia ndani mthili ya mwizi. Wahaka ukawa bosí wa kuamrisha kila jambo. Chibago hazina yake ya subira ikawa tupu.

Piiii!

Piiii!

Honi iliendelea kupigwa kwa kelele pale getini.

Agness akaingia ndani, akavua ile sketi iliyochafuka kisha kaitupa chini ya kitanda haraka na kuchukua khanga moja na kutoka nayo nje mbio. Akamfungulia mlango mshefa wake wa Kigogo. Usowe ulisema yote. Nambari kumi na moja imejichora vema kabisa. Ndita kazikunja mithili kalamba ndimu.

"Pole, mume wangu—kwa kucheleta kukufungulia," kijuso tena kilijawa na aibu bandia. Akaongeza. "Nilikuwa haja kidogo wakati umefika getini, na bahati mbaya mimi nd'o nilikuwa nafika kileleni!" Chevuu! Kama kaulizwa vile. Mshefa hakujibu kitu jambo lililomfanya Agness apate wasiwasi kuwa pengine ameonwa au kuna mtu amemuona na kumbonyeza mshefa, naye kaja kwa ziara ya kushtukiza tena amenuna na kuvimbiana kama bunju.

Alijikausha na kujisemea moyoni, "Mnhuu! Ngoja nitajua tu nisijipe presha ya bure. Na nilitumie lile kombora kuanza kumpima *hapahapa* nje." Mshefa alipitisha gari ndani hadi eneo la egesho lake. Kwa nyuma Agness akaufunga mlango. Katika dhima yake ya kutaka kumvuruga kisaikolojia mshefa wake,

akakibinua kiuno chake juu. Sio kwa kusudi alizokuwa akifanya. Khaa! Mungu anamwona kwa kweli. Mtegoni akaingia bwana mkubwa. Akamezea mate. Agness akafunga komeo la kati la geti huku mzigo ulioumbwa ukaumbika ukitikisika Singida Dodoma. Khanga moja tu iliyofungwa ovyo-ovyo kutokana na haraka alizokuwa nazo Agness ilitosha kumfanya mshefa ahisi nywele zinamsimama na roho kudunda kwa kasi kama mtu mwenye presha, aliuweka mkono wake wa kuume upande wa kushoto wa kifua chake na kusikia Gugum! Gudum! Gudum!

“Mama yangu hizi ndio zile presha za kujitakia!” Mshefa akajisemea moyoni huku akimkodolea macho Agness, domo amelizebua mwaaah! Akajiinua taratibu hadi pale mlangoni mwa gari ambapo mshefa wa Kigogo aliendelea kusimama kwa hamaki pasi na kujua afanye nini. Agness alipiga hatua fupifupi za madaha zilizokifanya kifua chake chenye vititi vidogo mtindo msumari vizidi kumkoroga mpenzi wake.

Alimfikia na kumpa bonge la busu la shavu, “Mmmmwaaah! Pole baby eh... nisamehe!” Agness alisema huku sauti ikiwa kama inatokea puan. Hata haisikiki thabiti. Chibago akameza funda la mate kisha kwa taabu akasema. “Usihofu, dear! Niko sawa tu. Hebu twende ndani,” Mshefa alisema wakiongoza njia ya kuingia ndani. Katika kurutubisha huba, Agness akampokea mkoba bwanaye. Tena kwa makusudi akatangulia mbele ili alitingishe wowowo. Akainua mguu kupanda ngazi ya kwanza. “Jamani! Jamani! Jamani Agness wewe!” Chibago alilia na roho yake.

Afanaleki! Wallah! Neema za Muumba zilipishana tena hizi zikipanda, hizi zinashuka. Akachanganya mwendo basi zile neema zikawa kama zinapiga makofi ama zipo katika maji zinabubujika kwa utepeto! Ashukuriwe Muumba kwa kuleta viumbi hivi na neema zake! Shefa huko nyuma halina hali kabisa. Hajamaliza hata kidato cha ngazi ya pili—amebaki

akilegeza tai huku pumzi zikikimbizana kama jogoo lililohemewa kwenye mapambano.

“Baby, baby! Polepole kidogo... unaenda kasi sana siwezi mie mwenzako kupandisha kama wewe. Naomba uje unishike mkono basi tupande sote!” Mshefa alisema kwa sauti nzito yenye kitetemeshi na mikwaruzo ya huba. Ni wazi mtego wa Agness ulikuwa umemnasa pabaya. Kama ni samaki basi ni ndoano imemnasa kwenye matamvua kabisa. Hana pa kupumulia.

“Bila shida, baby! Mimi na wewe tena!” Agness alijibu kwa sauti yake ya huba. Laitani nd’o ungekuwapo katika eneo la tukio na ukabahatika kumsikia Agness akiongea, basi ungetamani aendelee tu kuongea. Akashuka kidato kimoja cha ngazi ya pilii kutokea juu. Ua wake una ngazi tano pana sana. Alibakisha ngazi moja afike juu. Lakini kauli ya mahabuba wake ikamrudisha nyuma pasi na na kupenda. Akamkamata mkono wa kushoto wa mshefa wake na kuubana kwenye kwapa lake la mkono wa kulia. Mkono huo ukajikuta umebanwa na joto la kwapa la Agness na kuangukia juu ya titi lenye umbo la kifuu kukazaliwa fukto la kutosha mtimani mwa Chibago.

Akauhisi kama mkono huo umedumbukizwa kwenye maji yenye fukto la kusisimua. Mwili wote ukamtetema na suruali yake ikaanza kupata ujazo mkubwa kwa mbele. Mzee maneno yakaanza kumtoka palepale ngazini.

“Sijawahi kukuchoka kwa kweli... huu mwili ulioumbwa kwa asali haunishi hamu... utajiri wa tabasamu lake linanivutia wallah sijawahi kujuta kukupata!” Agness alibaki akitoa tabasamu lake lililojawa na stihizahi nyingi nafsini—kwani muda si mrefu ametoka kugawiana kile anachokigharamia shefa huyu na mwuza madafu. Katika kuchagiza maneno aliyoyasema bwa’ Kigogo Agness akasema.

“Acha masihhara, baby, basi!” Agness aliongea akimwangalia mshefa wake kwa jicho pembe. Mshefa akawa amebanwa na Agness huku akimfuata kama mbuzi

anayeperekwa kwenye kafara. Karibia mara alikuwa akitupa jicho lake mgongoni kwa Agness na kujaribu kuwa refa kati ya ile milima miwili iliyokuwa ikishindana kwa kuinuka kwa zamu kutaka mwamuzi aamue ni nani mkubwa zaidi.

Hamaki na udenda ulivyomshika, mshefa likamtoka neno pasi na na kuwa na hiya, “Ah! Soki oza na mbongo te basi kitoko bakotikela basemekina yo.”

Alijikuta akitamka maneno kwa lugha ya Kikongo kama alivyoyakariri baada ya kuyasikia kutoka kwa rafiki yake mfanyabiashara kutoka Kongo. Alipomwuliza rafiki yake maana ya msemo huo aliambiwa kuwa, “Kama huna pesa wanawake wazuri wataishia kuwa shemeji zako.” Sasa alikiri kuwa angekuwa kapuku kamwe asingewahi kuumiliki mchuma kama huo. Ya Mungu ni mengi! Ajabu mwuza madafu alikuwa kambamiza ukutani Agness. Laiti kama isingelikuwa kiwewe chake, basi yaliyotokea nje yangebaki ndani. Mdomo koma!

“Unasemaje baba Chanja?” Agness akajiuлизisha baada ya kumsikia mshefa akianza kuongea lugha zisizoleweka. Alijua ni kwa alivyomnasa kwenye wavu wake wa kokoro. Hatoki, hang’oki. Ana nini? Alitolee wapi. Thubutu yake! “Mhu, mhu!” Mshefa akatoa viguno viwili vyta kujibaraguza kuonesha kuwa hajiwezi hata kujibu swalii la bibie huyo mwenye umbo la kuvunja chaga. Agness akahamanika.

“Mbona hivyo, *baby*?”

“Hapana kwa kweli. Naona nachelewa kufika ndani ili nijipatie haki yangu,” Shefa alisema. Hata ikawa kama katiwa utambi huyo Agness tena kuchezesha makalio yake kwa makusudi ili kuongeza kasi ya mapigano ya moyo wa mshefa. Akambeba msobemsobe mshefa wake hadi ukumbini. Kwa uchovu na hamasa aliyopewa na Agness, mshefa akajipweteka sofani huku akivuta mkono wa Agness.

“Aih! jamani, *baby*, mwenzako!” Agness alipoona kavuta mkono, ndipo alipoendelea kujidekeza huku akijiangushaa

mapajani mwa shefa la Kigogo. Haki ya Mungu Agness anajua kutumia silaha ya jicho. Alilegeza kupita kiasi.

"Nini tena, Aggy, wangu. Nisamehe Sana! Leo umekuwa mawazoni mwangu tangu mchana. Tafadhali naomba utulize mtima wangu maana sina kipepeo kingine cha nafsi isipokuwa wewe!" shefa la Kigogo yalimtoka huku akifanya ziara kadha wa kadha maungoni kwa Agness. Hakumhini tena bozi wake aliyekengeuka mtima kwa hiyari. Akawa anasafirisha mkono wake kuelekea jikoni kwa Agness.

Hata fursa hiyo akampa basi? Safari haikumea hata mguu wa pili kufunguka, akamdaka mkono kisha akasema, "*baby, no, kwanza*. Ngoja. Nikamalizie kujisafisha halafu nirudi tena kwako. Usihofu hii yako lazima niitake radhu!" Agness aliendeleza kuboresha mahusiano yake na mtaji wake!

Akainuka mtoto wa kike mwendo kama anapaa. Taratibu hakuwa hata na pupa ya kufika huko aendako. Hatua ya kwanza huko nyuma mshefa presha ikampanda na kumshuka. Akaongeza kamwendo basi kama vile ndo' kachochea mapishano.. kuchu—kuchu—kuchu, loh! Hatari lakini salama! Akajikuta anahimiza pasi na kupenda. "Fanya haraka, *baby*, uvumilivu unakaribia kunitokea puan!" Mgogo yalimtoka akiwa amekalia bungungu. Hakuweza tena kukaa sawa sofani.

"Usihofu, hani! Naja sasa hivi," Agness alijibu kwa kisauti chake chembachemba.

Baada ya dakika tatu mbele, Agness akarudi na khanga nydingine moja nyepesi iliyolowa na maji huku ikishika maumbile yake kisawasawa. Akasogea hadi pale alipoketi mshefa kisha akainama kuwashaa TV. Mali zote zilibaki na nyuma na kuzikabidhi machoni kwa mshefa. Mlima mkubwa wa asili uliojiotea wenyewe kwa dhamira ya kuamsha walilala kumpa presha ya kujitakia sofani alipoketi bwana Chibago.

“Baby, njoo basi—mbona hivyo jamani!” Shefa la Kigogo lilihimiza. Kama alikuwa na ugeni na Agness. Ama kweli kupenda ni upofu.

“Nakuja, baby, ngoja nikuwekee mambo mazuri kwanza,” Agness alisema huku TV ikiwa inaonesha mkanda wa video wa mchezo wa matusi. Akarudi hadi pale alipo Mgogo. Akaanza kumshika polepole na kumvua viatu vyake alivyoingia navyo hadi sebuleni

“Pole, *baby* eh, ulisahau kuvua viatu!” Agness alisema kisha akamkandika busu la shavu la kulia. Shoti kali ya kihisia ukapita katika maungo ya Chibago. Ukipata unayempenda, mahaba, visa na mikasa ya kimapenzi havizoeleki. Moyo wake ulibaridika kupita kiasi. Atake nini zaidi ya starehe ya nausi aliyokuwa akiipata kutoka kwa Agness. Akasema.

“Usijali!”

“Usijali!” Shefa alisema huku pumzi zake zikiwa hazina ushirikiano. Mabega juu panda, chini shuka.

Agness hakusubiri aambiwe jukumu lake ni nini. Akaanza kazi ya kumbadili mtu kuwa kama alivyokuja duniani. Akawa mtupu babu wa watu kanyoosha miguu mbele kama anayesubiria kuchinjwa. Hana mamlaka hata punje. Mamlaka yote anayo Agness. Zaidi alikodoa macho pima. Hilo dogo. Katika kutaka kuhakikisha shefa limefikwa himayani mwake, Agness akampandia juu ya kiuno chake. Akatanabaisha yale aliyoyapokea unyagoni kwa ufundi bila papara. Matendo yakiwa yangali moto, mboni ya Agness ilikataa kwenda likizo kumtazama shefa. Aliyagandisha machoye akisaili kazi kubwa iliyokuwa ikipata makunyanzi ya shefa.

Kwa kiasi kikubwa mechii ilishikiliwa ipasavyo na Agness. Hakutaka kuonesha udhaifu au utofauti na siku zote afanyavyo. Alihakikisha hamuhini bwana Chibago kwa namna yoyote ile. Ndani ya hekaheka, Chibago alijikuta akisema;

"Sing'usuma ishi bila gwegwe!" kalima za Kigogo zilianza kusikika. Mdundo wa moyo wake ulipiga maradufu.

"Siku... elee...wi—*baby*, unasemaje?" Agness aliuliza huku akiendelea kukaanga mbuyu akimwachia mwenye meno atafune. Akaacha kuendelea kufanya kile alichokuwa anakifanya. Akamtupia jicho lililosheheni huba zito bwana Chibago. Akawa anamzaba vikofi vidogodogo vyatayi mahaba ili kuchachua ladha ya huba. Akasindikiza na mengine mengi ambayo mwandishi hawezu kuyasema. Raha zilizomzidia, wazimu ukampanda, akalombokeza;

"Gwegwe—mwana!"

"Gwegwe—mwana!"

"Gwegwe—mwana!"

Agness alimchezesha sindimba babu wa watu hadi kufika kipande cha Mawezi alikuwa hoi bin taabani.

"Pole sana, mpenzi eh! 'mechoka?" Agness alimwuliza mshefa wake kwa kauli ya udadisi na mahaba. Tabasamu safi usoni mwake. Akihemu akajibu; "Unauliza embe Kibada!" Naye akatoa tabasamu kusindikiza furaha yake.

"Umekuwa Mzaramo, bebe?"

"Kwanini?"

"Hayo mambo ya Kibada umeyajulia wapi?"

"Aah jamani, Agness. Nimekuja DAR mwaka 1976 Chuo Kikuu. Unadhani Siwezi kuujua mji kweli mpaka sasa?"

"Hapo kweli! Sijazaliwa bado!"

"Aah kumbe we' mwanangu kabisa eh?"

"Wewe tena huyo?"

"Mimi ndiyo. Mwanangu wewe wa kuzaa kabisa!"

"Nyoo! Mwanao ungenilala, una wazimu nini?"

"Mekutania bebe!"

"Nalijua hilo. Na mimi nimekutania!"

"Mmmhh!"

"Unaguna nini sasa? Hivi unajua pamoja na urefu na ukubwa kiumri, lakini mkiwa kitandani nyote mnakuwa kimo na umri sawa. Upo?" Agness alimjibu mshefa wake huku akiangua kicheko. Kwa pamoja walifurahia maisha yao ya kimahaba kisha Agness akainuka na kwenda kuutaka radhi mwili wake mnono wa kupendeza. Alijiokota polepole na kumtambuka mshefa aliyeonyoosha miguu yake kwa uchovu. Alikuwa amelalia mgongo huku akisikilizia umeme wa kihisia uliokuwa ukiuchoma kwa furaha na huzuni moyoni mwake.

Usiku mrefu wa malavidavi kwa kati ya Agness na mshefa wake ulikwisha. Kama ilivyoada kwa watoto wa kike, alimwandalia mpenzi wake kifungua kinywa. Akapata alichostahili. Bwana akatoa shukrani kemkem kwa pishi la Agness. Alisindikizwa kwa maneno matatu mezani hapo kisha akaaga. Maisha haya ya kuja na kuondoka kwa bwana mshefa imekuwa kawaida sana. Hukaa huko akaapo, akijisikia kuja, pengine angebadili gia angani, akamghilibu mkewe kama yu safarini ghafla, na kutua katika kiwanja cha alichomjengea Agness.

Kwa wizi wa Agness, akamsindikiza mpaka nje kabissa akatoka ndani ya jumba la geti. Mshefa nyumba kaijengea Uswahlilini makusudi ili aje kujificha mahali ambapo itakuwa si rahisi kuhisi ama kudhani kama ana nyumba. Uswekeni kabissa konakona zimetawala. Huyo Agness sasa akiwa nje aliquwa akimpungia mkono bwanaye wakati akipotea taratibu machoni mwake.

Akatazama majirani zake wasichana wadogo-wadogo wengi wanaomchukia kwa tambo na kusudi zake. Agness hawakumzidi uzuri wa sura na shepu, hata ki-uwezo utofauti wao ulikuwa ardhi na mbingu. Kwa fujo zake za mtaani, amejikuta akiingia magomvini pasipo kupenda.

SEHEMU YA PILI

“Loh! Yule mwanamke anajisikia balaa! Sijui kama kasalimika mzee watu kupewa ndogo,” sauti ilisikika kutoka eneo la mbali kiasi kutoka kwa wasichana watatu waliokaa kibarazani wakimtzama Agness akiagana na mshefa wake. Ajabu iliyioje, Agness alikuwa akifanya yake kwa dhamira ya kuwarusha roho majirani zake wanaodanga na kuishia kupata pesa za chips na vijora tu mtaani hapo. Hakuvumilia. Aliwasikia vyema kabisa. Akasema.

“Mtasema sana... kama ndogo ni mali na nyie si mtoe tuone?”

Lahaula! Kawasikia. Walidhani mambo yao yalikuwa kizani, kumbe kule kujitia kumuaga mshefa dhahiri shayiri ilikuwa danganya toto kwa peremende lakini nadhari yake yote ilikuwa kwa wasichana hao walioshonana kwa makundi kibarazani kwao. Hawakumudu gharama za kununua ukimya. Yakawatoka.

“Kwenda bibi we! Kazi kuua kwa watoto wa watu kwa UKIMWI tu hapa mtaani!” binti wa pili alimjibu Agness akirusha mikono kwa ghadhabu.

“Kama tatizo ni nyota, bonyeza reli!” Agness alijibu akichapa mkono wake wa kulia mapajani kwake.

“Kwendraaa! Usitushu lishe sie ‘apa!’” Binti alijibu tena kwa hamaki kubwa. Vumbi la maneno likapambana moto.

Agness akageuka kwa hasira na kuwatazama kwa jicho la kuwahuksudu mno. Alikuwa kavaa kanga moja rangi nyeupe iliyoadikwa “Alaa Kumbe!” na nakshi za visuvisu. Katika kutaka kuleta hamaki ya mtaa, afriti mkubwa akajitia kama a’taka kuokota kitu. Macho makinifu kuelekea kwa wale wasichana.

Kengele ya hadhari ikawaka, wakaanza kukaa vyema kwa hofu ya kutupiwa mawe.

Wakati anataka kuinuka, akaanza kupigisha makofi maumbile yake ya nyuma kwa mtindo usioelezeka. Yakawa kama yanatetema. Loh! Khanga nayo kwa kimbelembele chake, ikaanza kuzama katika pachipachi ya makalio. Kisha akapiga hatua moja mbele na kurudi nyuma mithili ya mtu anayechenza kiduku. Astaghfirullah huo msambwanda ulivyokuwa unarindima na kutoa mihemo huko nyuma ni hatari tupu.

"Kama mnaweza na nyie fanyeni! Mtaishia..." akasema neno linalohusiana na kujamiihana. Akaongeza, "Bure mtaani 'apa hadi nyuke zichakae hizo. Wapuuzi wakubwa nyie! Mch!" akamaliza na sonyo refu. Kwa hasira, akabamiza geti lake akiwa anarudi ndani. Salamu za upopo zilijidhihirisha baada ya mchanga kadhaa kuruka kutoka na kasi ya geti kufungwa.

"Hiloooo! Utajjuuuu!!!" wale mabinti waliongea kwa sauti ya pamoja. Wakamkera Agness akatoka tena nje. Akawatukana matusi mazito kuhusu nyeti za mama zao. Alisema maneno mengi ya kusugua nafsi. Alitamka kila baya na unango nuksi aliwaachia. Hawakuthubutu kurudisha matusi. Walikuwa kimya bila kusema kitu. Pamoja na jeuri yao, wanamjua kama Agness ni mwehu asiyesubiri mwezi mchanga kichaa chake kipande.

"Najua n'tawakomeshaje nyi' mbwa!" Agness alisema kwa kughadhibika mno. Usowe ulisema yote.

Baada ya masaa manne, Agness alitoka ndani kwake na kuelekea dukani. Kutokana na wivu wa mshefa wake. Aligoma kumwekeea mfanyakazi ndani si wa kike wala wa kiume. Anataka Agness abaki peke yake bila mtu mwingine ye yeyote ndani ya nyumba yake. Wakati anapita mtaani kwake, wale mabinti walikuwa uwani wanafua nguo na mvulana mmoja alikuwa amesimama akiongea nao. Kwa vile ana usuhuba mkubwa na ushari, hakuridhia kupita bila kuanzisha chokochoko. Akasema.

"Mambo, Davie!" Agness alimsalimia yule mvulana aitwaye Davie kwa sauti ya kimahaba. Davie hakujibu. Badala yake, akamgeukia msichana wake katika moja ya wale waliokuwa wanafua nguo. Msichana akamwonesha sura ya kukwazika na salamu ya Agness.

"N'nakutaka uitikie salamu yake!" msichana aliyejkuwa anafua alimtisha mpenzi wake. "Sio vyema, Sakina!" Davie alijibu. Hakuwa na hakika kama hilo lilikuwa sahihi kulisema au la. "Dokodoko!" yule msichana aliyetajwa jina la Sakina na Davie alijibu huku akibana pua zake na kurejea maneno ya Davie aliyyoyasema.

"Unamwogopa huyo kimbaumbau? Njoo ule supu hii!" Agness alijibu kimaudhi. Kwa kuonesha rangi halisi ya dhamira yake, akaendelea; "Kwanza nipeleke sokoni na gari lako, we' si' ni dereva wa Uber au hilo gari unapiga nalo picha tu mtaani na videm' vyako?" Agness aliongeza. Kusudi kuu likiwa kuchefuana nafsi. Aliwaona wasichana wa mtaani kwao hawana majabu. Watu wa kupitiwa na walala hoi wasiojua kutunza bali kumaliza haja zao. Pengine aliwaona hawajui kutafuta idhaa inayoonesha mwanga mzuri wa maisha. Basi tabu tupu mtaani hapo.

Wale wasichana wakafyumu. Yakaanza mazogo mithili ya majogoo ya sikukuu vile. "Weeeee!!! Ishia hapohapo! Koma kabisa! Tena ukome mshenzi mkubwa we!" Sakina alisema kwa hasira huku akishika kiuno chake na mikono akiipaisha.

"Nikome kwa lipi?"

"Hilo la kumshobokea bwana'ngu!"

"Nimemshobokea au hujui bwana'ko ka' mfanyabishara?"

"Kama sijui au najua, haikuhusu!"

"Hata kama, lakini huyo ni dereva wa Uber... ubanifu huo utakula nini?"

"Sio lazima pesa apate kutoka kwako, bibi we!"

"Kama angekuwa na kazi asingekuwa hapo anasogeka na wewe..."

“Koma! Hayakuhusu n’shakwambia!”

“Hayanihusu, lakini yananihusu. Davie twende unipeleke sokoni. Kama hataki turudi wote nyumbani ukachukue gari yangu tuondoke!” Agness alisema kwa msisitizo sasa. Safari hii alimsogelea Davie kabisa na kumshika mkono. Akaamshwa mbogo aliyelala. Hatari na nusu! Sakina akainuka pale alipo. Uso umewiva kwa ushari. Pumzi zinatoka puanı kwake hadi milango ikaonekana midogo jinsi alivyokuwa akihema. Kuibiwa bwana kuna mambo asikwambie mtu.

“Embu rudia tena kwanza nikusikie, umesemaje?” Sakina aliongea kwa hasira—kaivaaa suti ya ugomvi ilimpendez mno. Akauputa mkono wa Agness uliokuwa umemshika Davie kwa minajili ya kuianza safari.

“Achana na mimi... sina muda wa magomvi...” Agness alijibu kisha akageuka zake aondoke. Kabla hajapiga hatua ya kwanza alisikia nywele zake za rasta zimevutwa kwa nyuma kwa nguvu sana almanusura shingo yake ivunjike.

“Maamaa!” Agness alipiga yowe kali la uchungu.

“Niwache! Niwache we mbwa n’nakwambia!” Agness alifoka kwa hasira lakini haijasaidia kitu Sakina alienedelea kunyongorota nywele za Agness. Kutokana na urefu wa nywele zake, Agness alifanikiwa kijigeuza na kumzaba kofi moja matata sana Sakina la kinyumenyume—hadi kenda chini kuisalimia ardhi pasipo kutaka.

Bila kupoteza muda, Agness alijisogeza palepale chini alipodondoka Sakina kuisalimia ardhi kwa mfululizo wa makonde. Akaanza kumzaba vibao vya kulia na kushoto vile vya kelbu matata sana hadi kupelekea kumwumiza mashavu yake Sakina kutokana na pete aliyovaa Agness. Hakuridhika na makofi yale, akataka akunje ngumi ili ampige nayo, Davie baada ya kuona hivyo, akaingilia kati. Maana aliyekuwa chini aliquwa mwanamke wake. Kupigwa mbele yake halikuwa jambo la stara.

“Jamani eh! Jamani eh! Hebu acheni mambo ya kitoto,” Davie alisema huku akimshika Agness sehemu za kwapani alimoingiza mkono wake na kutengeneza kabali matata ya kumwinua Agness asiendeleze ugomvi wake na Sakina.

“Agness, inatosha basi. Acheni hii kitu kabisa!” Davie alifoka.

“Mwambie mwanamke wako awe na adabu na si mimi,” Agness alisema kwa hasira. Sakina aliendelea kujishika shavu lililovilia damu kwa makonde msokoto. “Nyoo! Na bado hiyo pati gazeti nimekupa!” Agness alisema huku akisukumwa upande mwininge na Davie. “Agness ‘ebu twende kwanza hiyo safari yako ili tuondoe hii shari kwanza,” Davie alisema huku akimsukuma Agness kuelekea katika gari yake. Sakina aliendelea kutweta bila kujua nini afanye. Agness akainama chini akaokota kikapu chake cha ukindu na kuelekea mahali ambapo gari ya Davie ilipaki.

Aliingia ndani ya gari kisha kufunga mlango. Davie kabla hajatoa gari, alisimama mlangoni na huku ufunguo ukiwa inaning’ia, akawambia mpenzi wake, “Nisubiri narudi sasa hivi—ngoja tuijepushe na huyu pepo!” akaingia ndani ya gari aina ya Passo na kutekenya ufunguo, injini ikakohoa safari ikaanza.

Davie na Agness hawakuongea chochote kile hadi wanafika sokoni. Walifika sokoni Agness alinunua mahitaji yake kisha akamrudia tena Davie. “Nenda tu, nitachukua gari nydingine. Ahsante kwa msaada wako,” Agness alimwambia Davie. “Hutaki tena safari? Utarudi vipi nyumbani kwako?” Davie alihoji. “We’ wala usijali. Unaweza tu kwenda!” Agness alijibu kishujaa. Davie akajikusanya kisha akaondoka zake.

Agness alibaki anabuzibuzi pale sokoni kama aliyekuwa akisubiri kitu au mtu. Akapita bodaboda mmoja, akamsimamisha na kuondoka naye.

Punde Davie akafika kwa akina Sakina. Sura za wale wasichana wote zilikumbwa na kisirani usoni. Ndita hasa!

“Habari zenu!” Davie alitoa salamu kwa wale wasichana. Hakuna aliyeitikia salamu yake. “Jamani nimesalimia—mbona kimya tena?” Davie aliongeza. “Bwana we”! Kwani huko ulikotoka salamu hazijakutosha tu?” Mmoja kati ya wale wasichana alijibu. “Zuleha embu tulia kwanza nimwonyeshe shoo huyu mrombo!” Sakina alidakia. “He! Shoo gani tena, Sakina?” Davie alihoji kwa wasiwasi. “Kwa hiyo umemwona yule malaya wako ndo’ wa maana sana kuliko mimi, sio?” Sakina alihoji kwa tashtiti. Tena mikono ikiwa imeshikamana na kiuno. “Hapana. Nimeiondoa shari iliyoianza,” Davie alijibu.

“Shari?” Sakina aliuliza kwa mshangao.

“Ndiyo, shari!”

“Inakuhusu nini we’ hiyo shari?”

“Ingepelekeea kuumia kwako!”

“Kwanini usinitoe mimi nikaondoka nawe, badala yake ukaondoka na yule changudoa, kwanini?”

“Niliona ndo’ njia pekee ya usalama wako!”

“Si kweli!”

“Kweli tena!”

“Basi haya kusanya virago wende zako kwako ukamwendeshe na makalio yake!”

“Usiseme hivyo, Sakina, mpenzi!”

“Ninasema vizuri kabisa!”

“Sakina, wewe!”

“Kwendaaa! Si umemwona yule wa maana. Sikutakii!”

“Usinifanyie hivyo, Sakina!”

“N’takwitia kelele za mwizi sasa hivi... ondoka! Ondoka!”

“Sawa, Sakina—mi’ naondoka!”

“Kwendraaa mwana kwenda!”

Sakina hakutaka kusikia visingizio vyta Davie kuhusu lile alilolifanya. Alishajazwa maneno na mashoga zake hakutaka

kusikia a wala be. Kinyonge, Davie aligeuka na kuelekea mahali gari lake lilipoegeshwa. Akiwa anakaribia katika gari, Agness naye akawa anapita na yule bodaboda aliyemkodisha akiwa kule sokoni.

“Davie, vipi?” Agness alisalimia.

“Ovyo tu!”

“Kwanini?”

“N’shaachwa kwa ajili yako!”

“Khaa? Ya kweli hayo?”

Davie akageuka nyuma kuwaangalia akina Sakina watasemaje. Badala yake, wakamnyari vilivyo. Midomo imebetuliwa chini juu, juu chini huku viuno vikinesa kwa maringo. “Nadhani unaona mwenywewe!” Davie alisema. Agness akashuka katika bodaboda. Akamsogelea Davie pale alipo.

“Pole sana, Davie” Agness alisema huku akitupa jicho la huba.

“Ahsante, Aggy!”

“Sasa utafanyaje?”

“Sijui kwa kweli... labda nimwache kwanza hasira zake zimwishe...”

“Haya, basi baadaye!” Agness aliaga kisha akamsogelea Davie karibu.

“Nini tena, Aggy?”

“Sogea karibu, Davie nikunong’onozee jambo fulani!”

Davie akasogea karibu... “Mmmwaah!” Agness alimshambulia busu kali la kimahaba shavuni. Wale visokorokwinyo wakaona. Wakaacha yao wakaanza kumwangalia Davie atafanyaje lakini Davie hakushituka—aliendelea kumwangalia Agness tu.

“Nipigie simu baadaye!” Agness alisema.

“Sina namba yako,” Davie alijibu.

Wakabadilishana namba mbele ya wale wasichana na wala wasifanye chochote kile. Baada ya hapo, Davie akaenda zake—Agness akaongoza njia ya kurudi nyumbani kwake.